**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE**

**Kumb. Na.HWK/S.1/24/Vol.III/** **05/10/2021**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi hizo. Tangazo hili limetokana na **Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb. Na. FA 170/369/01"B"/108 cha tarehe 15 Septemba, 2021** kilichotolewa na Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

## 1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III- NAFASI MOJA (1)

### MAJUKUMU YA KAZI.

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao; kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- Katibu wa Mikutano na kamati za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umasikini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiji.
- Mwenyekiti wa Kikao cha Wataalamu waliopo katika Kijiji.
- Kupokea,kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi;
- Kusimamia utungaji wa Sheria Ndogo za Kijiji; na
- Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

### 1.2 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu Elimu ya Kidato cha Nne (IV) au Sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo:- **Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

### 1.3 MSHAHARA

Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS.B kwa mwezi.

## 2. DEREVA DARAJA LA II - NAFASI MOJA (1)

### MAJUKUMU YA KAZI.

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- Kufanya usafi wa gari
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (IV) na mwenye leseni ya udereva ya Daraja la E au C1 ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

### 2.2 MSHAHARA

- Kwa kuzingatia Ngazi za mishahara ya Serikali yaani TGS.B kwa mwezi.

### NB: MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE:

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
3. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, maelezo binafsi, vyeti vya Kidato cha nne au kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa husika na Picha moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma. **Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.**
4. Waombaji wanatakiwa kuwa na namba ya Utambulisho wa Uraia kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA).
5. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na/au kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
6. **Testimonials "Provisional Results" Statement of results; hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) <u>HAVITAKUBALIWA.</u>**
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi; wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.

9. Uwasilishaji wa barua kwa Mkono katika Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe **HAURUHUSIWI.**
10. Waombaji wote watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili (Interview)
11. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoanishwa hayatashughulikiwa.
12. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **19 Oktoba, *2021*.**
13. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na barua ya maombi isainiwe na kuambatishwa na vielelezo vinavyohitaji na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:-

| | | |
|---|---|---|
| **Mkurugenzi Mtendaji,<br>Halmashauri ya Wilaya,<br>S.L.P. 584,<br>Korogwe.** | Au | **District Executive Director,<br>Korogwe District Council,<br>P.O. Box 584,<br>Korogwe.** |

**NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe www.korogwedc.go.tz**

Halfani H. Magani
**MKURUGENZI MTENDAJI**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
S.L.P 584
KOROGWE